OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA SIMIYU

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

Simu: 0764424802
0713251444
0735251444
E-mail:nassasecondary@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI NASSA,
S. L. P 440,
BUSEGA.

KUMB. Na. NSS/JIN/22/21 **TAREHE:…….**

MWANAFUNZI ……..

SHULE YA MSINGI ……

BUSEGA

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASSA WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.</u>

- **UTANGULIZI**

  Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Nassa ni ya kutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (Wavulana na Wasichana). Ipo umbali wa kilometa 2½ kutoka Nyashimo kuelekea barabara kuu iendayo Lamadi, Bunda hadi Musoma.

  Masomo yataanza tarehe **11/01/2021**. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe **18/01/2021.** Mwanafunzi asiporipoti ndani ya muda huo hatapokelewa shuleni.

- **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**
  - Sare ya shule:
    - **Wavulana:** suruali bluunyeusi (darkblue Namba 1) mbili zenye marinda mawili kila upande, mkunjo wa chini “turnup” mzingo kwa chini inchi 21.
    - **Wasichana:** sketi bluunyeusi (darkblue kitambaa Namba 1) mbili zenye marinda 14 tu zinazofika kwenye kifundo cha miguu (visigino)
    - Mashati meupe mawili mikono mifupi yawekwe alama ya kidato bega la kushoto kwa kutumia rangi ya kitambaa cha suruali/sketi.
    - Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.
    - Soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo na mapambo yoyote.

- Viatu na T-shirt ya bluu kwa ajili ya michezo na sweta la bluu kwa ajili ya baridi.
- **KWA WANAOVAA HIJAB.** Mashono ya nguo yazingatie maadili ya dini husika.
- Tai zenye michirizi ya rangi nyeupe na blue na nembo ya shule.

- Vifaa vya kujifunzia: Daftari kubwa 12, kalamu za wino, penseli, rula na mkebe wa hesabu (Mathematical set).
- Faili moja dogo aina ya **"folder file"** la rangi ya khaki kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
- Vifaa vya usafi.
  - Ndoo moja (lita 20) ya plastiki.
  - Ufagio mgumu wa plastiki (Hard Broom)

- **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

  Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

  - Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la **LAZIMA**.
  - Mahudhurio mazuri kwenye kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni **LAZIMA.**
  - Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
  - Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
  - Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
  - Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
  - Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
  - Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
  - Kutunza mali za umma.
  - Kutovaa mavazi yasiyo ya heshima.
  - Kutofuga kucha ndefu, na kutokuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
  - Wanafunzi kutumia lugha chafu wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine.

- **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- Wizi.
- Uasherati na ushoga.
- Ubakaji.
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi, n.k.
- Kupigana au kupiga.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- Kudharau Bendera ya Taifa.
- Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- Kuoa au kuolewa.
- Kutoa mimba.
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kukataa adhabu kwa makusudi.
- Kuwa na simu ya mkononi.

- **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**
    - Medical Examination form **"KIAMBATISHO B"** ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya **serikali**. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
    - Fomu ya maelekezo binafsi **"KIAMBATISHO A"** kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi/ mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
    - Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

EDWARD M. PETRO
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASSA

Kiambatisho "A"

MKATABA WA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASSA

ANUANI YAKO…….

.....

……

Tarehe……

Mkuu wa Shule,

Shule ya sekondari Nassa,

S. L. P 440,

BUSEGA

SEHEMU "A" (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

Mimi…….ambaye ni mvulana / msichana niliyekuwa nasoma shule ya Msingi……. wilaya ya ……. mkoa wa ……..nakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Nassa iliyopo Busega Mkoa wa Simiyu leo tarehe …… Nitazingatia sheria za Shule na za nchi hii, nitakuwa mwaminifu, mwenye bidii na juhudi katika masomo, kazi za nje na michezo.

JINA LANGU……SAHIHI……
TAREHE……

SEHEMU "B" (IJAZWE NA MZAZI / MLEZI)

Mimi……mzazi/mlezi wa ……ninayeishi kitongoji cha …….kijiji cha…….wilaya wa …….mkoa wa …….....nakubali mtoto wangu kujiunga na kusoma katika shule ya Sekondari Nassa kuanzia tarehe……. hadi atakapohitimu kidato cha nne. Mtoto wangu nitampatia mahitaji yote yanayotakiwa shuleni. Nitahakikisha kuwa ninafuatilia kwa ukaribu sana mahudhurio, mwenendo na maendeleo yake shuleni. Hivyo sintasita kumuonya na kuchukua hatua za kisheria pale atakapobainika kutenda lolote kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule ya sekondari Nassa.

Jina langu……
Sahihi…….
Namba ya simu……Tarehe……

Kiambatisho "B"

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
NASSA SECONDARY SCHOOL

PART A:

Full name (school child) ……..……

Age: ……height (cm) …….sex…….weight……

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for joining secondary school. The examination should include the following categories (I –III) each category or Sub category of which, will render the applicant ineligible in each of a defect. Pregnancy (Plano test), category IV will render a girl student ineligible.

- Eye – sight ……
- Hearing …….
- Speech ……..
- Venereal disease (HIV) ……
- Leprosy and T.B Disease …….
- Epilepsy ……
- Spleen ……...
- Chest/Abdomen ……
- Blood Coat …….(Red and White)
- Urinalysis ……
- Neuroses …….
- Additional information e.g. physical defects or impairments, infections, chronic or family/heritable diseases
- (eg sickle cell) inability to eat certain food etc.

  ……

  ……

- Pregnancy

  ……...

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named school child and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for Secondary Education course.

Name and signature ……..

Designation ……

Station …….